



USAWA WA KIJINSIA NA USHIRIKISHWAJI WA JAMII

Bomba la Mafuta Ghafi la Afrika Mashariki (EACOP) limeshamiri kuheshimu na kuzingatia haki za wanawake na sheria zinazotumika katika shughuli zetu na kazi za taasisi. Sera hii ya Usawa wa Kijinsia na Ushirikishwaji wa Jamii inafafanua na kuweka malengo ya EACOP kwa ajili ya manufaa ya wadau wote, wa ndani na wa nje.

Sera hii ya Usawa wa Kijinsia na Ushirikishwaji wa Jamii inawiana na Sera ya Haki za Binadamu ya EACOP ambayo inakataza ubaguzi kwa misingi ya asili, jinsia, umri, ulemavu, utambulisho wa kijinsia au yanayohusiana na hayo, pamoja na aina yoyote ya unyanyasaji, ajira za shuruti/kulazimisha kwa watoto (Sera ya EACOP ya Haki za Binadamu ya mwaka 2022). Pia inazingatia Mkataba wa Kutokomeza aina zote za Ubaguzi Dhidi ya Wanawake (CEDAW) (1979) ulioidhinishwa na Serikali ya Uganda mwaka 1985 na Serikali ya Tanzania mwaka 1986.

Kwa kuongozwa na Kanuni za Uwezeshaji Wanawake za Umoja wa Mataifa, EACOP inahimiza mazingira ya usawa na heshima, inachangia jitihada za kuwawezesha wanawake katika jamii pana, na kukuza utamaduni ambapo wanawake na wanaume wanapewa fursa sawa ya kujiendeleza na kustawi. Tunaamini kwamba usawa wa kijinsia si tu haki ya msingi ya binadamu bali pia ni kichocheo muhimu cha maendeleo ya kijamii na kiuchumi.

EACOP INAKUZA USHIRIKISWAJI WA KIJAMII NA KUZIBA PENGO LA JINSIA WAKATI WA AWAMU YA UJENZI NA UENDESHAJI. EACOP INA AHIDI.

- Kutambua umuhimu wa dhamira na utendaji wa uongozi unaowezesha usawa wa kijinsia ndani ya kampuni kupitia usawa wa kijinsia, ushiriki wa kijinsia na uongozi wa wanawake. Uongozi wa kampuni ya EACOP utaendeleza usawa wa kijinsia katika ngazi zote za kampuni, ikiwa ni pamoja na uwakilishi wa bodi na vyeo vya juu katika usimamizi.
- Kukuza utamaduni wa kampuni unaounga mkono mahali pa kazi pasipokua na ubaguzi, ambapo wafanyakazi wote wanatendewa kwa heshima na kupewa fursa sawa za kukua na kujiendeleza.
- Kulinda afya, usalama, na ustawi wa wafanyakazi na waajiriwa wote wanawake kwa wanaume, kutambua majukumu ambayo wanaume na wanawake wanaweza kuwa nayo kama walezi katika kaya.
- Kusaidia kukuza maendeleo ya wanawake kitaaluma ndani ya kampuni kupitia mafunzo na ushauri, kuwawezesha wanawake, vijana na makundi mengine yaliyo katika mazingira magumu kupata fursa mbalimbali za kuchagua na kufikia uwezo wao kamili.
- Kusaidia maendeleo ya shughuli za uzalishaji, mnyororo wa ugavi, na shughuli za manunuzi yanayoenda sambamba na Sera hii ya Usawa wa Kijinsia.
- Kuchangia usawa wa kijinsia katika jumuiya pana kwa kushiriki kikamilifu katika mbinu za kuelimisha, mipango na ushirikishwaji unaokuza usawa wa kijinsia, na unaosaidia mtaji wa kijamii katika mitandao ya wanawake. Tunadhihirisha unyeti kwa muktadha wa kijamii na kitamaduni ambayo tunafanya kazi.
- Kufanya kazi kwa uwazi na uwajibikaji kwa kupima na kuripoti Viashiria muhimu vya Utendaji
- Kwa wafanyakazi wetu ndani ya kamouni na washirika wetu wa shughuli na wakandarasi walioko uwandani kuhusu maendeleo.

Utekelezaji wa sera hii umeandaliwa katika MPANGO KAZI WA JINSIA wa EACOP na unategemea kupitiwa mara kwa mara na Kamati ya Uongozi ya Haki za Binadamu na kuhuishwa kulingana na dhamira ya EACOP ya uboreshaji endelevu. Tunatoa taarifa kwa serikali wenyeji na wadau wetu kuhusu dhamira yetu ya kuheshimu haki za wanawake. Sera hii inatumika kwa wafanyakazi wote wa EACOP. Tunawahimiza washirika wetu wa shughuli na wanakandarasi kutenda kwa namna inayoendana na kanuni zilizowekwa katika sera hii.